SWAHILI FORUM 12 (2005): 37-62

MAZUNGUMZO NA LUTZ DIEGNER JUU YA RIWAYA YA *ZIRAILI NA ZIRANI*

WILLIAM E. MKUFYA

William E. Mkufya aliyezaliwa mwaka 1953 wilayani Lushoto, Tanga, nchini Tanzania ni mmojawapo wa waandishi wakongwe wa riwaya ya Kiswahili. Hadi hii leo amechapisha riwaya nne. Aidha, ameandika vitabu kumi na viwili vya watoto na kutafsiri baadhi ya vitabu, kama vile riwaya ya *Kiu* ya Mohamed Suleiman Mohamed. Riwaya za *Ziraili na Zirani* na *Ua la Faraja* zimeshinda Tuzo ya Fasihi ya Kitaifa Tanzania katika kiwango cha Muswada Bora wa Riwaya mnamo 1999 na 2001. Katika mazungumzo haya yaliyofanyika tarehe 29 Januari, mwaka 2004, huko TYCS, Upanga, Dar es Salaam tulitia mkazo zaidi kwenye riwaya yake ya kiepiki *Ziraili na Zirani* (1999). Hapa na pale mwandishi kaelezea riwaya yake nyingine *Ua la Faraja* (2004) iliyokuwa haijatoka wakati ule. Hivi sasa mwandishi ni mhariri katika kampuni ya uchapishaji *Mangrove Publishers*. Alikuwa katibu mtendaji wa Baraza la Maendeleo ya Vitabu Tanzania (BAMVITA) kuanzia 2002 hadi 2004. Anaishi Dar es Salaam. Hivi sasa yumo mbioni kuandika riwaya iitwayo *Maua Nyikani* ambayo itakuwa juzuu ya pili ya trilojia atakayoita *Maua* ambayo ilianza kwa *Ua la Faraja.* Juzuu ya tatu itaitwa *Ua Limenyauka*. Mwandishi anakusudia kutafasiri riwaya zake za Kiswahili kwa Kiingereza.

Lini na kwa nini ulipata mbegu ya kuandika Ziraili na Zirani?

Sasa, unajua, nina hadithi ndefu kuhusu lini na kwa nini niliandika riwaya hii. Kuandika *Ziraili na Zirani* ilikuwa ni lazima ningeiandika, ila mimi mwenyewe nina historia ya muda mrefu kuhusu mtazamo wa imani. Kwa hiyo lini? Ni mwaka 1981, tuseme hapo ndiyo nilipoanza kuiandika hiyo *Ziraili na Zirani.* Niliiandika kama hadithi ya kurasa mia moja tu. Lakini kabla ya hapo nilikuwa na mtazamo wangu kuhusu imani, na nilikuwa najua tu, siku moja nitaandika kazi itakayosema ninavyoamini mimi. Unaona?

Kwa hiyo kuanza kuiandika ni mwaka 1981 tuseme. Nikaiwasilisha. Kuna rafiki yangu mmoja alikuwa anafanya kazi hapo *Oxford University Press*, alikuwa anaitwa Anthony, Anthony Majengo. Sasa yeye akaipeleka Chuo Kikuu na profesa mmoja akaisoma aka-*comment* kwamba ni nzuri sana na inachokoza mawazo ya mtu. Lakini wakati huo ilikuwa inazungumzia tu, *incidence* ya mtu mmoja alivyofariki, alivyofika kuzimu na akawa na matatizo katika kujikabidhi kwenye hukumu. Baada ya pale yale maoni yaliyotolewa na yule Profesa, nikayarekebisha nikaiandika upya. Sasa…

…alikuwa profesa yupi?

…nadhani alikuwa Prof. Mbunda. Sina uhakika. Huwa wasomaji wa miswada hawapendi kuacha majina yao yajulikane kwa mwandishi. Sijui kwa nini. Nikarekebisha yale aliyoelekeza. Nilivyokwisha kuyarekebisha nikaipeleka *Oxford University Press* Nairobi. Kule alikuwepo mhariri wa siku nyingi sana, sasa hivi ni marehemu. Anaitwa Brian Hocking. Basi yeye, ile kazi ikamfurahisha sana. Ikamfurahisha, akampa mhariri. Kawaida *publisher* akishasoma

muswada anawapa wasomaji wa ziada walioko nje ya ile kampuni wausome muswada kisha watoe maoni yao. Akampa.

Nadhani huyo aliyepewa muswada ule alikuwa mtu mwenye imani kali. Kwa hiyo akaikatakata kwa wino mwekundu, akasema… ninazo zile nakala za maoni yake. Lakini yeye amenisaidia sana. Yale maoni yake yalikuwa makali, na kwa hiyo *Oxford University Press* wakasema hawawezi kuichapisha. Lakini yeye hajui kwamba alinisaidia sana kwa yale maoni yake, kwa sababu nilijua kwamba nikiandika bila kuwa mwangalifu, itawaathirije wale wenye imani ya namna ile. Kwa hiyo nikawa nimepata nafasi ya kujieleza zaidi.

Halafu yeye, Mzee Brian Hocking akaniuliza – kwa sababu hata wakati nilivyokuwa nikiandika, nilikuwa nimeshasoma Dante na Milton. Lakini Milton, *Paradise Lost*, nilikuwa sijaielewa vizuri, kwa sababu ni utenzi mgumu, hata *Divine Comedy* ya Dante pia niliuona mgumu. Lakini nilikuwa nimezipitia tu kama kijana, nikazielewa nusunusu. Kwa hiyo akaniuliza umezisoma hizi? Nikamwambia nimezisoma. Akaniambia kazisome tena. Kwa hiyo nikaenda nikazisoma tena.

Sasa nikawa mimi mwenyewe nina msimamo wangu. Wakati ule nilikuwa na mtazamo wa Kimarx, kwa hiyo baadhi ya hoja za Milton kwenye *Paradise Lost*, hasa pale, nadhani ni Raphael, anapomuusia Adamu, sikukubaliana nazo. Unaona? Bado hadi leo sikubaliani. Lakini ile sanaa, ile *epic handling* ya hizo hoja na matukio nilikuwa nimezifurahia sana. Kwa hiyo akaniambia kazisome tena. Ndiyo nikaanza sasa kuzisoma na ndipo nikaanza kuandika upya ile kazi. Ni kama niliichanachana na kuiandika upya kabisa. Ule ulikuwa ni mwaka 1981.

Baada ya mwaka huo nikaenda Budapest, Hungaria kwenda kusoma *glass technology* kwa muda wa miezi tisa. Wakati huo nilikuwa nafanyakazi NDC. Kwa hiyo nikawa sijapata muda wa kuendelea nayo. Nilivyorudi nikawa fundi mkuu wa kiwanda cha NDC cha kutengeneza chupa kwa ajili ya hizi *tube lights* na balbu. Lakini sasa huo muda ukaniruhusu nikitoka kiwandani napata muda wa kusoma fasihi na falsafa kwa umakini zaidi.

Kwa hiyo katika hicho kipindi cha karibu miaka minane nafanya kazi *Light Source Manufacturers Ltd* nikawa naendelea tu kusoma falsafa na kuzidi kujiimarisha na *Marxism* kuiangalia *from the other angle* pia. Kipindi kile wafuasi wa Umarx walikuwa wengi. Ni muda mrefu, nimeiandika kwa muda mrefu.

Na ulimaliza mwaka tisini na nane, kwa sababu ilitoka tisini na tisa?

Ee. Nilimaliza tisini na nane kui-*typeset* na nini... Lakini ndiyo kwenye tisini na nane hiyo nilimaliza. UWAVITA walinifadhili. Walinipa shilingi laki nne nikaenda kijijini kwetu kuiandika upya. Kwa ujumla, nimeiandika karibu mara sita: yaani naandika, naandika upya, naandika upya – zaidi ya mara sita. Kwa hiyo hata kila neno la ile riwaya nimelichagua. Si kwamba yameangukaanguka tu kwa kusimuliwa! A-a. Yaani kila mstari au sentensi imekaguliwa kwa umakini na umantiki, ili kuwe na muunganiko wa msuko wa matukio.

Umekusudia kumfikia nani kwa riwaya ngumu kama hiyo?

Kwa kweli sikutaka, sikukusudia iwe ngumu, ila yale yanayoongelewa kwenye riwaya ya namna ile ni magumu. Kwa hiyo mimi mwenyewe ningependa iwe rahisi sana. Na ndiyo utaona kwamba hata Kiswahili nilichotumia nimefanya makusudi kiwe chepesi, mtu yeyote anayekisoma, aweze kukielewa kile Kiswahili. Kitakachomtatiza ni zile *concepts.* Yale mashauri yanayojadiliwa mle ndiyo yatakayomtatiza, lakini ni kwamba nilitaka nihadithie kwa lugha inayoeleweka kwa kiwango kikubwa.

Lakini baadhi ya maneno ya msamiati pia ni magumu kidogo, au unafikiri watu wanaoitwa wa kawaida wanayaelewa yote?

Msamiati – ndiyo sababu nakwambia mle kila neno limewekwa kwa sababu lilingane na hoja au tukio. Kama utakuta neno gumu lina sababu ya kuwekwa mle, kwa sababu neno lingine la rahisi lingerahisisha ile dhana iliyoko mle ndani. Si kwamba nimetumia neno gumu kwa makusudi tu ya kum*bombast* mtu, a-a, ni kwamba likiwa mle, lina sababu ya kuwemo mle. Na siyo mengi sana hata hivyo.

Je, katika kumuumba mhusika Zirani, ulimchanganya na maisha yako?

Ndiyo. Ndiyo. Zirani, unajua, kile kichwa cha ile riwaya ni *Ziraili na Zirani*. Yule mtu anaitwa Fikirini Zirani. Ndilo jina lake. Kuzira Kiswahili ni kususa. Kwa hiyo nawaambia watu kwamba: Fikirini mzire! Mkifikiria haya mambo ni heri mzire. Ni heri msusie, msusie hizo dini, kwa sababu haziwasaidii. Ndiyo jina lake yule Fikirini Zirani.

Nimemchanganya na maisha yangu kwa kiwango fulani, kwa sababu mimi nimekuwa natatanika sana kuhusu hizi imani. Kwa muda mrefu nimekuwa nazira. Hivyo, kama nilivyokueleza, kwamba nimekuwa nazitazama na naona kwamba kwanza zinaathiri maisha ya watu, nazo zenyewe zinaji-*contradict.* Lakini bado watu wanalazimika kuwa nazo, halafu hawana jinsi yoyote ya kuziepuka. Hili ndilo tatizo kubwa.

Tunaweza kusema kwamba mada kuu ya riwaya hiyo ni uchunguzi wa dhana ya dini pamoja na mikinzano inayotokana na waumini na wasioamini, na mikinzano baina ya waumini wa dini tofauti. Hapo umetia mkazo kwenye dini za Uislamu na Ukristo. Ulikusudia zaidi kuzingatia mikinzano baina ya dini hizo mbili, au lengo lako lilikuwa kuijadili misingi ya dini zote?

Ukifika kwenye ile sura inayohusu vita ilipokuwa inapiganiwa kule mbinguni, unaona nilijaribu kuwaita wote, hata mashetani wa Kihindu, mashetani wa Kizoroaster, niliwahusisha mle. Kwa maana ya kwamba ile vita ni vita yote ya jamii yote, na ya jamii zote za kibinadamu zinazoamini.

Kwa hiyo, maana yangu hapo ni kwamba ninakusudia kuzisema dini zote zinazoamini uungu. Ila kwa sababu hadhira yangu mimi ni ya Waislamu na Wakristo, hapa eneo letu la Afrika Mashariki, Afrika kwa ujumla na sehemu kubwa sana ya ulimwengu, hadhira yangu kubwa zaidi ni ile, halafu mimi mwenyewe sijawa na ufahamu wa kutosha kuhusu dini za mashariki ya mbali, za Kihindu, Kibuddha, na hizi nyingine, kwa mfano za Japani. Kwa hiyo kama ile riwaya ingeanza kuzijadili hizo ingekuwa mbali mno na hawa wasomaji. Ningeanza

kwa mfano kuweka miungu ya Kishinto au imani za Kishinto, au hekima za imani ya *Confucius*, riwaya ingejitenga mno na hawa wasomaji wa kawaida. Kwa hiyo ni heri nilivyozijadili zile ambazo tunazo japokuwa kusudi ni imani zote kwa ujumla.

Mawazo mawili makuu yanayopingana katika riwaya hii yanawakilishwa tayari katika madondoo ya mwanzoni mwa riwaya. Wazo la kwanza la Mfalme Ashoka linasema kwamba dini zote ziheshimiane na kwa kuheshimiana huko, zipevuke na zipevushane. Wazo la pili la Bertrand Russell linasema kwamba uwingi wa dini tofauti unadhihirisha kwamba hakuna hata dini moja iliyoweza kuwa kweli. Anaongeza kwamba msingi wa dini yoyote ile ni woga.

Katika riwaya yako tunasoma dondoo lifuatalo juu ya asili ya dini yoyote ile: "Woga huu unapopevuka unabatizwa na kufinyangwa kimantiki na falsafa na kuitwa dini." (ZZ Motoni V). Ukiangalia hayo mawazo mawili makuu ya mwanzoni, wewe uko upande gani?

Mimi yale mawazo mawili yote nayapenda, kwa sababu usitegemee hoja moja kutekelezwa mara moja – labda kwenye mapinduzi – lakini kama unataka *transformation*, *social transformation*, inaenda kwa ngazi. Kwa hiyo kikweli kwa hivi sasa, hali tuliyo nayo, hoja ya Mfalme Ashoka ni nzuri, kwamba sasa hivi ni upuuzi kuanza kukatana mapanga kwa sababu ya tofauti ya Mkristo na Mwislamu zile imani zinapotofautiana. Sasa ngazi ya pili ya *transformation* ya binadamu ni ile hoja ya Bertrand Russell.

Ukiniuliza nakubaliana na lipi ni vigumu kusema kwa sababu hiyo ni ngazi. Hatuwezi sasa hivi kuiambia jamii – imeshaathirika. Tumekuwa wagonjwa, yaani jamii ya Kitanzania na Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla, *infact* dunia nzima, ni wagonjwa, wameathiriwa na huo ugonjwa wa imani. Na tukiita dini ugonjwa, tutawaudhi watu. Huko nyuma dini ilikuwa na manufaa mengi hasa ya maadili. Hatuwezi kuyapuuza. Lakini kwa sababu sasa hivi dini zinapoanza kukaribiana na kugongana huleta madhara mengi, basi unaweza kuita imani: *ugonjwa*.

Kule nyuma kote labda imani hazikuwa ugonjwa, ilikuwa ni lazima mtu awe na imani. Lakini sasa hivi imani za dini ni ugonjwa. Sasa hatuwezi kuponya huo ugonjwa kwa dawa moja ya ghafla na kusema: "Acha!" Ni kama leo baada ya tatizo la ukimwi ukiwaambia watu "Msifanye *sex*!" Wameshakuwa watu wa utamaduni wa ki-leo, utamaduni wa kisasa. *Sex is part of the way of looking at life*. Sasa huwezi kuwaambia "Acheni!" Itakuwa kama wako jela.

Kwa hiyo ni lazima uanze labda kuwashawishi waanze kupunguza, kupunguza, kupunguza – hatimaye waone ni upuuzi kama anavyoona mhusika Alyosha wa Dostoyevski akiwa na Grushenka kwenye *Brothers Karamazov*, kwamba kuendekeza ngono ni upuuzi. Haina maana, haina manufaa, kama *it's just a playing around*! Lakini kwa hivi sasa ukiangalia televisheni, na vijana wanavyochangamkia *sex,* huwezi kutoka tu ghafla ukawaambia "Acheni!" Kwa hiyo ndivyo vile hata na hizo imani.

Lakini nafikiri kuna tofauti baina ya jambo hili na jambo la dini.

Bahati mbaya nimeihusisha na kitu ambacho dini zenyewe zinakichukia.

Ngoja, katika *Ua la Faraja* ninazungumzia tatizo moja – hilo neno *sex*. Katika *Ua la Faraja* ninazungumzia ukimwi, lakini dhamira mojawapo ni kwamba: tuiheshimu *sex.* Na kuiheshimu *sex*, siyo kusema ni kuiacha, au siyo kusema ni mbaya na kuiita shetani, au vilevile si kuitukuza na kuifanya kama riadha! Uliniambia kwamba nimelinganisha vibaya msukumo wa kuendelea na imani na msukumo, katika nafsi za mwanadamu, wa kuendekeza *sex*; yaani ile *analogy* haifai. Sasa ndiyo nikakwambia kwamba mbona na hizo imani zinaiogopa *sex*?

Kwa sababu sasa hivi kwa Mkristo au Mwislamu *sex* ni kama shetani yaani *sex* ni kama jitu, kitu kibaya sana. Katika *Ua la Faraja* nasema kwamba *sex* ni kitu muhimu sana kwa mwanadamu na ni kitu *sacred*, ni kitu cha kuheshimika, cha kutukuka. Sisi Waafrika kikwelikweli tunaitukuza *sex.* Si kwamba tunaitukuza kwamba tunaifanya mno... *fanatically*, a-a, yaani tunaiheshimu. Ni kama ni *sacred thing.* Na ukienda kwenye majando na unyago, wanafundishwa hivyo – yale ya asili, siyo ya sasa hivi, kwa sababu yale ya sasa hivi yameathirika pia na ile *sexist fanatism*. Lakini yale hasa ya jadi, zamani, yalikuwa yanatukuza *sex* kwa sababu ndiyo njia pekee ya kufanya jamii iendelee, idumu isipotee.

Kwa hiyo kile ni kitu cha kutukuza. Kwenye imani za Kikristo na za Kiislamu *sex* inaogopwa mpaka inakuwa kama yenyewe ina uovu ndani yake. Naona sasa tumeenda pembeni ya mazungumzo yetu.

Tukirejea kwenye Ziraili na Zirani: Katika riwaya hiyo, umetumia wahusika wengi na kutaja majina mengi sana, hasa ya wanafalsafa na mashujaa wa kihistoria kutoka dini mbalimbali (tz. ZZ Dhahara IV&V). Jambo hili halirahisishi usomaji wa riwaya. Halafu umeyarudia baadhi ya hayo majina mengi katika sura nyingine (tz. ZZ Mzingo wa Vita IV). Kwa nini umetumia majina mengi namna hiyo?

Ile riwaya nimekusudia kuwa na muundo wa *epic*, kwa hiyo *approach* au staili yake ya uandishi ni hasahasa ile. Siyo *epic* katika hii *modern concept* ya *epic* kwamba unaweza kuwa na *prose epic*. Lakini nilijaribu kutumia ile ile *style* aliyoitumia Vergil kwenye *Aeneid*, Milton kwenye *Paradise Lost*, na kadhalika, ambapo mashujaa au waoga hutajwa kwa majina yao yale yale.

Epic inazungumzia – hata zile za nyuma – ina uhusiano wa karibu sana na tukio la kweli. Ni masimulizi kuhusu kukabiliana na jambo na kumsifu aliyeweza kukabiliana nalo mpaka akaliweza. Yule aliyekabiliana na jambo, kama ni jambo dogo, tena la kwake pekee, sasa nd'o unapata zile *epics* kwa mfano za Homer. Ni kwamba yule mkabilianaji na hilo jambo ni huyo mmoja. Odysseus anakabiliana na vita, vita yake, halafu anapata masaibu, anakabiliana nayo, anayaweza.

Unapotoka kwenye ile *primary epic* ya akina Homer, unaingia kwenye *secondary epic* kama ile ya Vergil. Kwenye *Aeneid*, ni taifa la Urumi lilivyoweza kuhama kutoka hapo lilipokuwa mpaka lilipokwenda kuji-*establish* nchi ngeni*,* humo njiani likiwa linapambana vita na kukabiliana na matatizo mengi. Sasa pale hawezi kuwepo shujaa mmoja. Ni mchango wa watu wote kufanya hilo jambo liwezekane, au siyo?

Halafu unapoingia kwenye *secondary epic* nyingine, hiyo ya Milton, pia hayo maanguko ya mwanadamu yalielemezwa mno kwa Adamu. Ingawaje Adam alikuwa ndiye mhusika mkuu, tena wa pekee. Na hayo masaibu aliyokuwa anapata Edeni, yeye mwenyewe *as an individual*, na jinsi yalivyomwangusha. *Actually* kwenye Milton mimi huwa nasema kwamba "Ah! Kwani? Ni kweli Adam?"

Maana'ake inakuwa kana kwamba kulikuwa na vita kati ya mashetani na malaika huko jehanamu. Hapakuwa na vita, ila kulikuwa na maanguko ya Adamu kwenye *Paradise Lost.* Maanguko ya Adamu, alivyoweza kushawishika na shetani kwa kupitia kwa Eva. Lakini mle kwenye masimulizi aliyopewa Adamu kuhusu kilichotokea pia wanatajwa wahusika wengi, miungu ya Mesopotamia mingi imetajwa. Imetajwa miungu ya Misri, wametajwa watu mbalimbali, muhimu katika historia ya theolojia ya magharibi.

Mimi naona hii ni kawaida ya *epic*, kwa mashujaa kutajwa kwa majina yao. Na kusema kweli jambo ambalo ninalishughulikia kwenye *Ziraili Na Zirani*, ni jambo muhimu na nyeti kuhusu suala tata la dini – umuhimu wa kuwa au kutokuwa nayo. Linahusu watu wengi katika historia. Kwa hiyo ni lazima niwahusishe wengi ili hoja zangu ziaminike na ziwe na uzito. Kesi sharti iwe na ushahidi.

Unapokosoa dini inadhihirika kwamba unatia mkazo zaidi kwenye kukosoa dini ya Kikristo. Kwa nini?

Kwa sababu mimi mwenyewe nilikuwa Mkristo, na nilizaliwa katika mazingira ya Kikristo. Kabla ya sababu ya pili, inabidi kwanza niwasifu Wakristo. Pengine ni kwa sababu wamepitia katika *process* ya *intellectual development, intellectual transformation* ya muda mrefu kwa hiyo walishazoea kustahamili hoja zinazowasuta.

Halafu pili: Waislamu ni wakali! Yule mwanamke wa Bangladesh aliyeandika kuhusu haki za mwanamke zinavyoathiriwa na sheria za dini hiyo, ingawaje ametoa hoja za msingi kabisa lakini alipata matatizo makubwa. Kwa hiyo nayo pia ile imesababisha nisiwe muwazi sana kwa maoni dhidi ya Waisilamu. Niliisoma Qurani na kuielewa kiasi, kabla sijaandika hiyo *Ziraili na Zirani*.

Kwa hiyo kusudi halikuwa kwamba niwachambue Wakristo peke yao. Kama utaitazama ile riwaya hii leo, utakuta kwamba Wakristo wamewekwa kwa kuwakilisha dini zote..

Katika sura iitwayo Dhahara unasawiri dilemma ya kimsingi ya binadamu kuwa amegawanyika baina ya hiari na haja. Tunasoma dondoo lifuatalo: "tamaa haziepukiki japo zinatawalika" (ZZ Dhahara V 107). Unafikiri kweli kwamba dilemma hiyo ina suluhisho lililoweza kutawaliwa na hekima kiasi hicho?

Hiyari, haja, na hekima. Freud aliyatenganisha: *The Ego, the Id (which stands for the Libido), and the Super-Ego.* Si ndio hizi? Hata yule Hazrat Ahmad[1] aliyeanzisha *Ahmadia Movement*

[1] Hazrat Mirza Ghulam Ahmad. 1966. *The Teachings of Islam*. Rabwah: Tashbir Publication, Ahmadia Mission Pakistan. [First English translation published by Ahmadia Movement in Islam, Washington D.C. in 1953.]

anazizungumzia kwenye *The Teachings of Islam*, na yeye amezitenganisha. Anaziita nafsi *i-amarah*, nafsi *i-láwama* na nafsi *i-mutmainna*. Lakini zinakaribia kufanana na zile ngazi za Freud kuhusu nafsi ya mwanadamu. Nafsi *i-amarah* ndiyo hiyo *Ego*, na nafsi *i-láwama*, na-dhani ni hiyo *Id*, na nafsi *i-mutmainna* pengine ndiyo *Super-Ego*.

Kusudi hasa la kusema hivi ni kwamba hizi zote ni dhana kuhusu muundo wa nafsi ya mwanadamu. Muundo wake ni kwamba una sehemu hiyo inayohusu haja ambayo ndiyo *the libidinous part of* mwanadamu. Halafu iko hii sehemu ambayo inahusiana na hekima – *any-way* tuache kwanza hekima – inayohusiana na busara zake, yaani *the rational part*, halafu kuna ile ya hekima. Unaona? Huo muundo wa nafsi uko hivyo.

Sasa kuhusu swali lako linalohusiana na hilo dondoo: "Tamaa haziepukiki lakini zina-tawalika": Inawezekana! Ukienda kwenye ile sura ambapo Zirani ameingizwa kwenye ile kambi ya mashetani, kwenda kwenye *training*, wakawa wanajadiliana. Halafu ule muhutasari wa mafunzo yake kule akaueleza jinsi alivyoelimishwa na mashetani.

Sehemu moja ya ile hoja ni kwamba mwanadamu anaishi muda mfupi mno. Mwili wake una tamaa, lakini zinatawalika kama akili ikikua, busara ikikua. Lakini muda wa kukua busara ni mfupi. Kwa hiyo unakuta kwamba jamii zile ambazo watu wake wana muda mfupi wa kuishi, kwa mfano miaka sitini, hata busara za ile jamii zinakuwa ni changa na hafifu. Hata ile mifumo yao ya maisha inakuwa bado michanga na ghafi. Jinsi mwanadamu anavyoweza kuishi miaka mingi ndivyo atakavyoweza kutawala hizo tamaa. Mifumo ya kuishi ya watu wenye busara ina uwezo mkubwa wa kuwanufaisha watu kuliko ile ya watu waliopungukiwa na busara.

Mojawapo ya tata za misingi ya dini tofauti kama inavyotajwa katika riwaya yako ni kwamba waumini wanaamini kwamba kwa chochote wanachokitenda duniani, watahu-kumiwa mbinguni (tz. ZZ Zirani VI). Binadamu angeamini zaidi kwamba atahukumiwa papa hapa duniani, asingetenda kama anavyotenda. Unaona suluhisho gani kwa tatizo hili?

Kwamba atahukumiwa mbinguni – mimi siamini hivi. Hakuna kuhukumiwa mbinguni. Kwa hiyo la muhimu sasa hivi ni kuipondaponda hii hoja nyingine. Ni kuwaelimisha tu wanadamu kwamba huu ni upuuzi. Pa kuishi ni hapa hapa duniani.

Mimi naona kuna umuhimu wa kuwa na kosmolojia mpya. Kosmolojia inayozingatia ufupi wa maisha ya hizi nafsi na tatizo la utu wa nafsi. *What is religion*? Kusudi ni ile ile ya kuta-mani *immortality*. Kusudi ni kujenga hofu ya *mortality,* na kuzusha matumaini ya *immortal-ity, an imaginary immortality, which is not there.*

Sasa la muhimu ni kuweza kuukubali na kuustahamili ukweli kwamba tunakufa. Lakini kikwelikweli hatufi! Na hiyo ndiyo hoja ya *Ua la Faraja*. Hiyo ndiyo dhamira kuu kama ni-taifikia kwenye hiyo ngazi ya tatu ya *Maua*. Lakini nitawezaje na mazingira magumu ya uandishi? Bado naona kama sitaweza kufika mwisho wa hoja yangu. Jinsi ya kufika huko, sijui kama itaniathiri vipi.

Hoja yangu ni kwamba kwanza mwanadamu ameshajua, ameshaanza kujua au kukubali ukweli kwamba hakuna huko mbinguni tulikokuwa tunakutamani hapo zamani. Hata watoto wadogo wameanza kuupuuza. Unaona? Ni hatari! Kwa sababu, bahati nzuri nimeikuta humu kwa Dostoyevski, yule mmoja anasema kwamba mwanadamu akishaanza kukataa kwamba kuna *immortality*, hapo anaweza kufanya uovu wowote anaoutaka. Kwa sababu sasa haogopi mbele.

Ni kweli kwamba kuna hatari hiyo kwamba sasa hivi jinsi tunavyokaribia kuelewa ule ukweli kwamba hatuna usuluhisho mwingine tunaweza tukaingia kwenye janga kubwa la kutisha, na ile *absurdity* itakuwa *very very elevated*. Na watu watakata tamaa, watafanya mambo ya ajabu kabisa. Sasa kwa nini tusitafute *solution?*

Bila shaka usharika wa wanafalsafa utazua mbinu ya kupoza hatari ya kuzuka kwa janga la namna ile. Ng'ombe hajutii kuwepo kwake, hajutii kuendelea kulishwa na mwanadamu halafu atiwe kisu naye, auliwe, anyanganywe maziwa yake na mtoto wake, halafu anaenda kuuzwa huko. Hajutii. Tatizo la mwanadamu ni ile *reflective consciousness*, ile kujua, kujitambua na kujidadisi. Tumeshajitambua. Kwa hiyo *we have the challenge*.

Kwenye ile *Ua la Faraja* nitatoa mapendekezo ya suluhisho. Sitazisema sasa hivi, kwa sababu ziko katika kuumbwa. Sitaki kuzisema mpaka niwe na uhakika nazo. Kwa sababu nikizisema kama sijawa na uhakika nazo pia siyo sahihi.

Kwa tashtiti fulani inatajwa katika riwaya yako kuwa dini za ulimwengu zinachukulia kwamba asilimia tisini ya binadamu ni watenda dhambi, kwa hiyo motoni ni pahala pa uvundo mkubwa panapojaa tele (tz. ZZ Motoni I). Ungetathminije athari za dhana ya dhambi kwa historia ya binadamu?

Dhambi. Labda dhambi niseme ni uovu, kwa sababu dhambi ni kama jambo linalostahili adhabu vile. Yaani ukisema dhambi, una maana kuna hakimu - Mungu. Unapoanza tu kusema dhambi ina maana kwamba unaenda kinyume cha sheria fulani zilizowekwa.

Kwa hiyo mimi huwa silipendi hilo neno 'dhambi'. Kwa sababu sitaki kuwe na kitu kama hicho, mtu aliyeweka sheria, yaani Mungu au kitu kingine, ila ifahamike tu kwamba mtu kwenda kinyume cha mfumo itakuathiri. Ile *karmic vision* ya Kihindu au ya Kibuddha kwamba ukienda kinyume, athari utaipata; ukienda sahihi, furaha utaipata, au siyo? Sasa dhambi huwa si neno ninalolipenda zaidi. Napenda 'kwenda kinyume cha mfumo'. Labda ligundulike neno bora zaidi, au sheria, *law of nature*, kitu kama hicho, ambayo kwenye Kiswahili hatujaipata hiyo. Kwa hiyo liwepo neno bora zaidi.

Ndiyo. Lakini ile dhana ya dhambi, watu wengi wameishikilia na wameitathmini sana, halafu hii ilikuwa na athari kubwa nafikiri.

Ni sahihi kabisa. Ile dhana kwamba ni dhambi imewaathiri. Kwa mfano kuogopa kufanya jambo kwamba ni dhambi. Hata kuikosoa tu ile dini ni dhambi. Sasa huwezi kuikosoa. Kufuru ni dhambi, kwa Waislamu na Wakristo. Lakini kufuru ni kutokubaliana na zile desturi za ile imani. Sasa ina maana itakubidi kuogopa hata kukashifu.

MAZUNGUMZO NA LUTZ DIEGNER JUU YA ZIRAILI NA ZIRANI

Mengine zamani yalikuwa yakiitwa dhambi, lakini sasa hivi si dhambi tena. Kwa hiyo ime*suppress*. Hata hii *enlightenment* ya *the age of reason* ya akina Diderot na Descartes ni kwamba walianza kuonekana kama wao ni watenda dhambi, ni watu wabaya, wanaanza kusahihisha. Ndio wanaanza kusema hata yule Galileo alipoanza kuona zile nyota pia walianza kuona kama ni dhambi, ni kufuru. Kwa hiyo, hiyo dhana ya dhambi imesababisha sana ku-*suppress* upana wa kufikiri.

Ukikosoa dini, hasa zile ziabuduzo mungu mmoja tu, linajitokeza suala la dini barani Afrika: Ukristo na Uislamu zote mbili zimeletwa na wageni. Kwa kutoa mfano wa Kinjeketile unaonesha jinsi ambavyo alisilimu kijuujuu, lakini bado anamwabudu mungu wake Bokelo (tz. ZZ Motoni IV).

Tunaweza kuhitimisha hoja mbili: Ama nafasi ya imani za kijadi itambuliwe ipaswavyo na wakuu wa dini za Ukristo au Uislamu, ama Ukristo na Uislamu ziachwe kwa sababu hayahusiani na utamaduni wa kiasili wa Waafrika. Ungependelea hoja ipi binafsi, na kwa Waafrika kwa ujumla?

Katika hiyo sura kuna mahali ambapo Kinjeketile anaambiwa na Zirani na wenzake walioenda kumtembelea kule motoni "Sasa acha!" Kwa sababu walimwuliza maswali "Mbona huyo Mungu wako haji kukutetea huko huko motoni?"

Mwishoni kina Zirani wanamwambia Kinjeketile, "Basi, jiunge na sisi tuachane na mambo ya imani." Kuna mmoja mle kuzimu walimwambia hivyo akawatukana na kuwafukuza. Lakini huyu Kinjeketile akawaambia "Nendeni nifikirie". Sasa wakaondoka. Alivyofikiria jibu lake alileta lini?

Ile riwaya imeungamana, hakuna sehemu ambayo haina *connection* na kwingineko. Kwa hiyo unapokuja kwenye hii vita utakuta kundi la Kinjeketile likaja vitani. Kwa hiyo kama lilikuja vitani ina maana alikubaliana nao. Ndivyo ilivyokuwa kule vitani shetani akawa anawatania, anawaambia "Na nyinyi mnaokula nyama za vidudu mmekuja hapa!?"

Lakini ndivyo hivyo inavyojidhirisha kwamba na yeye Kinjeketile amekubali kuingia kwenye hiyo vita ya imani zote kuzipinga. Hiyo ndiyo sababu kwamba nilikuwa upande wa Kinjeketile kuhusu imani za Kiafrika. Lakini sasa Kinjeketile naye kukubali – maana yangu ni kwamba hata hizo za Kiafrika pia si muhimu. Ninachosema ni kwamba hapakuwa na sababu Waafrika waletewe imani nyingine. Hapakuwa na sababu. Na ni haki kabisa kwamba Kinjeketile alikuwa anasema "Hatukuzisilimu uchi. Nilisilimu nikiwa tayari na vazi langu la hadhi."

Kwa hiyo kule kuletwa kwa imani nyingine hapakuwa na haja. Lakini hata hizo za Kiafrika zilizopo sasa kwa hoja ya sasa hivi nazo hazina umuhimu. Ndiyo sababu ya lile kundi la Kinjeketile, pamoja na kwamba lilikuwa linataka imani zao za asili ziheshimiwe, na wao wenyewe waliamua kujiungana na vita. Ina maana kwamba na ile ya kwao pia wameikana.

Sasa hii zaidi ni hoja yako kama mtu binafsi, au ungependelea kwamba Waafrika wote wangefikiri hivyo? Tukisema katika siku za karibuni au katika hali ya sasa hivi, unafikiri inawezekana kweli kwamba Waafrika watambue jambo la kwamba tuache dini zote – zikiwa za jadi au zisizo za jadi, haina tofauti – tuziache zote, au ni kama hatua ya mbele?

Kwanza hiyo riwaya si kwa Waafrika peke yao. Hiyo ni *a universal epic.* Kwa hiyo kusudi si Waafrika peke yao. Na ndiyo sababu nasema kwamba hata wale wa Kinjeketile walijiunga kwenye ile vita maana yake ni *a human problem*, siyo *problem* ya Mwafrika peke yake. Ingawaje historia ilivyowapitisha ni kwamba wao walienguliwa, walinyimwa nafasi ya kuonyesha imani za kwao, kama vilevile Waskandinavia walivyoathiriwa na Wayahudi. Si Waskandinavia ni Wakristo sasa hivi? Lakini, si hii ina maana kwamba imani ya Kimesopotamia imeenda kule? Si ndiyo hivyo? Au Wajerumani pia, na Wataliano na kadhalika? Si wote wameletewa ile?

Jinsi Waafrika walivyo na tatizo ndivyo walivyo nalo Waitaliano, Wahispania, Waingereza, Wajerumani, wote wana hilo hilo tatizo kwamba ni *a Mesopotamian faith* imeenda mpaka kule kwao. Tatizo ni kwa watu wote. Lakini Mwafrika sasa hivi akisema "Mimi narudia dini za jadi", sasa ni kwamba ameruka mkojo amekanyaga mavi! Kwa hiyo sasa hivi itakuwa ni *absurd*, itakuwa ni ujinga na kichekesho kurudi na kuanza kushika pembe ya uganga, na kuanza kuiuliza maswali ili ikutatulie matatizo yako… Haina tofauti! Schopenhauer naye anasema hivi kwamba hana tofauti yule ambaye ni Mkristo, na yule ambaye anaabudu mizimu. Hakuna tofauti.

Jambo linalohusiana na swali lililopita ni kwamba tamaduni za Kimagharibi zinatambua na kuhusudu kwa kiasi fulani tangu zamani dini nyingine za dunia kama Ushinto, Utao, Uhindu na nyingine, lakini hawazitambui sembuse kuziheshimu dini na imani za kijadi za Kiafrika (tz. ZZ Mzingo wa Vita IV). Unafikiri kuwa licha ya ubaguzi wa rangi vilevile kuna phenomenon kama ubaguzi wa dini?

Kikweli ni kwamba unaposema hivi sasa kwamba wanaziheshimu imani za Mashariki: wanaofanya hivyo sasa hivi ni wale Wazungu wa Magharibi wa leo...

... lakini imeanza zamani. Hata akina Goethe kwetu Ujerumani, na wengine wameanza zamani sana kufanya utafiti kuhusu hizi dini za Mashariki, kuzipenda sana na kuziheshimu sana kama utamaduni mwingine. Lakini kumbe kuhusu dini na imani barani Afrika hakukuwa na kitu kama hicho, kulikuwa tu kwamba "Ah! Ni upuuzi. Tusambaze Ukristo, basi."

Kwanza tukubaliane kwamba, mfano sayansi, kuna kwingine ambako ilipewa nafasi ya kuendelea na kukua vya kutosha, kuna kwingine ilikuwa *suppressed*, kuna kwingine… – na kwa hiyo, huwezi kusema kwamba utafiti wa kisayansi katika dunia uko katika usawa mmoja. Ni kwamba kuna kwingine kulikuwa na mazingira yaliyoziruhusu zipanuke au zirefuke zaidi. Au si ndiyo hivyo? Basi hata hizo dini.

Kuna dini ambazo zilipevuka kuliko nyingine, na hiyo inahusiana na maendeleo ya binadamu kwa sababu, kwa mfano upevu wa Ubuddha, hata Ukristo unaweza ukakwama. Uki-

taka ushindanishe upevu wa Ubuddha uko juu sana. Au ukichukua tu hata upevu wa Uislamu, kwa sababu Mwislamu kaanzia pale Mkristo alikoishia, akapata nafasi ya kupevuka zaidi. Ukiangalia zaidi utakuta ni kana kwamba Qur'ani imepandia kwenye mgongo wa Ukristo.

Kwa hiyo Wakoloni walivyotukuta sisi, ni kama walivyoenda Amerika Kusini, si waliwakuta watu kule, walikuwa na tamaduni zao pevu kama Wainka. Pengine walikuwa na miungu yao, au siyo? Waliwafanyaje? Si wale pia waliwatukana, waliona kwamba walichoamini ni upumbavu?

Inaonyesha kwamba heshima waliyo nayo watu wa magharibi kwa hizi imani za mashariki ni kwa sababu walikuwa wameshangazwa na upevu wake waliouona. Kwa mfano, na bahati ikawa ni *age* ya *enlightenment* ndiyo hasa walipoanza kuwa na hiyo *curiosity* ya namna watu wa mashariki walivyoabudu. Baada ya akina Descartes kuanza kutilia mashaka imani zao wakaanza kuuheshimu ule upevu wa imani za mashariki. Hata nao akina Schopenhauer walipoenda kule, na wao walianza kuyasoma yale waliyasoma wakiwa tayari wameshaanza kukubali kwamba tunaweza kujiuliza maswali ya hii imani.

Sidhani kwamba tunaweza kusema kwamba imani za Kiafrika hazijapevuka. Nafikiri katika kesi nyingi tatizo ni kwamba hatujui mambo mengi kuhusu imani hizo.

Sasa nilikuwa sijamaliza. Ndiyo sababu. Mimi ninapozungumzia upevu wa Ubuddha siushabikii kwa sababu yoyote. Au ninapozungumzia upevu wa imani za Warumi, sipendelei kwa sababu ya kwamba ni ya Kirumi. Au kwa mfano ninapozungumzia upevu wa imani za Uchina, nina maana kwamba imani hiyo ina ubora wake ambao uko kwenye kiwango ambacho kinaweza kunufaisha hata mitazamo ya kisasa kuhusu maisha, inakupa *logical solutions* au *logical possibilities*. Inakupa uwezo wa kukabiliana na mambo yenye utata. Mfano *Ying yang* inakupa vichocheo vya fikra vya hali ya juu – sasa Waafrika pia wanaweza kuwa wana vichocheo vya aina yake. Mimi hapo sikatai. Ni kama ninavyosema kwamba watu wa Amerika Kusini, wanaweza kuwa na *schemes of thought*. Lakini pengine hazikuwa zina*develop*.

Lakini kujibu hilo swali lako ulilouliza ni kwamba ubaguzi wowote unapokuwepo, yule anayebaguliwa, lolote alilo nalo linalomhusu linabaguliwa. Pakishakuwa na ubaguzi, nikishakubagua Luti, kwa hiyo chochote utakachosema nimekibagua, nimekipuuza, maana nakubagua kwa kukuogopa usinikaribie. Chochote unachosema nitakibagua.

Ni kweli, lakini India *imekuwa* colonized *pia. Na hawajabagua Uhindu kiasi hicho. Na swali jingine ni: hudhani kwamba imani za Kiafrika pia zilikuwa zimepevuka sana, lakini hatujui – sisi Wazungu hatujui – vya kutosha? Na hatuwezi kutathmini au tuseme ni vigumu sana kupata vigezo vya kusema huu ni upevu, na ule si upevu. Nakubali kwamba tunakuta upevu mkubwa kwa mfano katika Ubuddha, lakini kwa nini katika imani za Kiafrika tusiseme kuna upevu mwingine?*

Unajua mimi mwenyewe hapa nilipo ukiniuliza, juzijuzi tu ndipo nilienda nyumbani kwa kusudi la kimila. Mwaka juzi, nikaenda nyumbani kuhakikisha kwamba *ritual* fulani imefany-

ika. Kulikuwa na *ritual*, tuna *ritual* inayoitwa *'Fika'*. Sasa nilikwenda kushirikiana na wazee kuhakikisha *Fika* hiyo imefanyika, kwa sababu siku nyiingi sana ilikuwa haijafanywa. Mimi kwa kushirikiana na baadhi ya wanandugu tukachanga pesa ili kuhakikisha yale mahitaji yote yanayohitajika, ng'ombe, vyakula, vimepatikana. Kweli tulifanikiwa. Ile *Fika* ikawezekana kufanyika.

Nikiangalia kusudi halikuwa kushiriki peke yake, kwamba mimi pia nina imani ile ile, ndiyo sababu nikataka ifanyike. Si hivyo tu. Kusudi pia lilikuwa kupinga kutofanyika kwa *Fika* ile. Na pia kupinga kwamba Fika ile iliachwa kufanyika kwa sababu ya Uislamu au Ukristo. Kwa hiyo nikachangia kuhimiza mpaka ikafanyika. Bahati mbaya sikuwa na kamera ya video, lakini nilichukua picha. Sasa hivi naandika, naandaa maelekezo mafupi kuhusu jinsi ya kuifanya ile *Fika* ili hata watoto huko baadaye waweze kuirudia kuifanya. Kwa hiyo mimi ukiniuliza imani za Kiafrika – mimi mwenyewe sizijui! Kwa sababu ziliachwa kufanyika muda mrefu.

Hata hao wataalamu wa kisasa wa kisomi wa sasa hivi wanaotetea Uafrika, hata wenyewe maskini hawaujui, kwa sababu wameshatenganishwa na Uafrika wao halisi kwa muda mrefu. Wazazi wao, au kuanzia kizazi cha juu, *generations* tatu zimeshapita, hawa*practize*. Pengine, kama unavyosema, pengine zilikuwa zimepevuka. Pengine zilikuwa zimepevuka. Hata kama hazikuwa zimepevuka, ni nani alitakiwa kuzipevusha kama si Waafrika wenyewe? Kama kwa mfano umesoma *Facing Mount Kenya* ya Jomo Kenyatta, wana *rituals* ambazo wanazifanya, *and I think the Mau Mau spirit* ilikuwa na msukumo mkubwa sana wa kitaifa uliotokana na *Gikuyu cosmology*.

Kabla ya vita baina ya waumini na wasioamini pamoja na mashetani kuzuka, Zirani anaota ndoto ambapo mzee anamweleza kwamba aikubali tu ulimwengu kama unavyoumbwa, asijaribu kuufahamu (tz. ZZ Mzingo wa Vita III). Baadaye, Zirani anaifikiria sana ndoto hiyo. Je, katika yaliyosemwa na mzee, yamo maoni ya mwandishi mwenyewe?

Kwa kiwango fulani. Kwa sababu ya tatizo la imani yenyewe, halafu tatizo hasa la *kuwa* kwetu, *existence*, ni fumbo gumu. Fumbo gumu. Na kwamba tulifikirie, ni lazima tulifikirie, kwa sababu tuna-*exist.* Kwa hiyo ni lazima tulifikirie. Tulifikirieje? Hilo ndilo swali. Na tulilifikirieje ili lituathirije?

Hilo ndilo tatizo. Lakini kwamba tukilifikiria tutapata *solution* yake, ni ngumu. Na ndiyo maana ninavyosema ni kama sisimizi aliyeko kwenye msitu wa nywele kwenye kichwa cha Luti. Yeye ule unywele anaupanda kama mnazi halafu umwulize, "Luti ana sura nzuri au mbaya?" *[vicheko vikubwa]* Yaani atakuwa hakuelewi kabisa, hata umwelezeje, hata karne ngapi umweleze hatakuelewa kwamba haiba ya Luti ikoje. Hawezi kukueleza.

Sasa ndiye yule mzee anavyomweleza yule mwota ndoto, kwamba: Ni heri tu mlikubali umbile lenu. Mkubali uumbwa wenu. Na mnaweza kuamua kuabudu. Kuabudu kusudi lake si kwamba unamtukuza yule aitwaye muumba. Isiwe hiyo! Kusudi lisiwe kumtukuza ili mpewe zawadi ya mbingu au ya paradiso, a-a. Kusudi ni kwamba mpate *a system* mweze kuwa na

format ya kurahisisha maisha yenu, ile *existence* yenu ya muda huu mfupi ipate umaana na urahisi. Muweze kuiendesha iwe bila vikwazo, na iwe na furaha kidogo. Isiwe na matatizo mengi kama vita na nini. Kwa hiyo kusudi la kule kuabudu iwe hiyo, ku*create a certain schedule*, *a certain format, a certain system, a certain pattern of life.*

Zaidi ya hayo, mwishoni mwa riwaya Zirani anaishia kumwita Mungu (tz. ZZ Kiama III). Je, ulitaka kusema kwamba binadamu hata akijitahidi kwa nguvu zake zote kumkana mungu, atakapokuwa hatarini ndipo atakaporudi kwake?

Unajua swali hilo aliniuliza Profesa Madumulla. Akaniambia "Riwaya hiyo, Bwana wewe, umeianza riwaya yako vizuri". Hata Privatus Karugendo anayeandika makala kwenye gazeti la *Rai*, na Madumulla wakaniambia, "Wewe umeanza hiyo riwaya, sisi tunajua wewe ni *revolutionary*, ni *materialist* na *Marxist*, sasa imekuwaje kule mwishoni ukaingia kwenye *idealism* tena? Umejisaliti kwa kurudi kwenye *idealism*".

Nikamwambia Privatus Karugendo ambaye ni padri, "Bwana, unajua? Tatizo la mwanadamu ni kwamba anakufa. Halafu anapokufa hatima ya hapo baada ya kufa inaweza kuwa ni *obvious* kwamba ni *zero*, eh?" Sasa hiyo *zero* yenyewe *is a phenomenon* yenyewe, yaani kwamba kuwa *zero – can you imagine, you, Luti, to be zero*? *[kicheko]* Ni *absurd*?! *It's quite absurd.*

Nitakuwa zero *tu. Minyoo watanila.*

Likija bomu hapa likalipuka. Baah! *And suddenly you are nothing!* Sasa tunapofika hapo hakuna mwenye jawabu. Hata sasa hivi tunasema unazaliwa unakufa, basi, hakuna *postmortal existence*. Lakini sasa ku*approach* ile *zero* yenyewe inaudhi sana. *It's quite uncomfortable.* Halafu kufikiria kuwemo kwenye *zero* yenyewe inaliza au siyo? *[vicheko]*.

Mimi nawafikiria minyoo. Watakuja na kunila.

Kwa sababu unajua yule Meursault, mhusika mkuu wa *The Outsider* ya Albert Camus, alipokuwa anaenda kunyongwa mwanzoni alikuwa hilo jambo lilikuwa halimsumbui sana. Sasa anakaribia kwenda kunyongwa, ikawa inamsumbua. Mwanzoni alikubali kwamba yuko *existentialist* – lakini sasa anapozidi kukaribia... Kwanza, mchungaji akija kutaka amsalishe anamfukuzia zake mbali kama Bigger Thomas wa *The Native Son* ya Richard Wright. Pia yule kijana alipokuwa akija mchungaji kumsalia anamwambia "Kwenda zako sitaki kukusikia!" Unaona?

Ni kwamba haoni sababu. Anaamini kwamba hakuna *afterlife*, la sivyo asingemkataa mchungaji. Kama angekuwa muumini kweli, si angekubali aendelee kusalishwa ili akiri tu makosa yake aweze kuingia mbinguni? Sasa amejua kwamba hamna mbingu. Lakini bado ilikuwa ni tatizo kwake mpaka mwisho wa ile riwaya kwamba ana*approach the zero*. Hiyo ni tatizo tupu!

Sasa kumwita Mungu. Mungu si Mungu Mkristo, Mungu Mwislamu au mungu kitu chochote. Maana yangu ya hiyo "Ni mimi kwa kuwa ni mimi" niliyonukuu kwenye *Ziraili na*

Zirani ambayo nimeitoa kwenye bibilia ni hilo fumbo lisilo na utatuzi. Ile *phenomenon* ya ku*approach zero* ipo *whether* kwa kuitabiri kwamba mbele kuna maisha, au kwa jinsi yoyote ile, au kwamba ni sifuri yenyewe kabisa. Lakini tuikubali kwamba ipo na tuwe na mfumo, au jinsi yoyote ya kukabiliana nayo bila kufadhaika kiasi cha kuweza kuiruhusu i-*boomerang against the system, i. e. the existing world.*

Iki*boomerang* ina maana watu wanapo*approach* uzee wataweza kuanza kupiga watu ovyoovyo tu, kwa sababu wanajua wanakufa. Wanaweza kuyatia sumu maji ya mto wakawaua watu wengine. Kwa hiyo ni lazima tu-*create* kitu, *system* ambayo itakuwa *tranquilizer* ya hiyo *situation*.

Katika riwaya yako tunamkuta mwanafalsafa Voltaire akizungumza juu ya kuwepo kwa Mungu mmoja tu, juu ya uraia wa kidunia na kuwa dunia ni kama kijiji kimoja tu (tz. ZZ Motoni VI). Je, hapo Voltaire amekuwa mtabiri wa uwezekano wa utandawazi kuwa kitu kizuri?

[vicheko vikubwa] Uwepo utandawazi usiwepo – hata huo utandawazi tulio nao sasa hivi: una-*take advantage* ya mawasiliano ambayo yamerahisishwa sana. Lakini imerahisishwa kwa kiwango gani? Kwa sababu kuna ile *level* ya *science*, wanasema baadaye wataweza ku*cross the border to exist in two places at the same time.* Pengine inafikika.

Anyway – dunia tangu hapo ni kijiji kimoja. Hata kabla ya hii *modification* ya *communications* zetu. Bado dunia ilikuwa ni kijiji kimoja, ila hatujawa na muda wa kukitazama kama kijiji kimoja! Kwani dunia ina ukubwa gani wa ajabu kama utafikiria ukubwa wa *cosmos* au hata wa hiyo mbingu moja (*galaxy*) tuiitayo *Milky Way?* Kadunia ni kadogo tu! Ni kwamba tulikuwa wavivu wa kuitazama dunia kwa udogo huo. Sasa hivi tunapata nafasi ya kuweza kuitazama kama *one unit*.

Huyu Voltaire kusema alikuwa mtabiri – hatukuwa hata na haja ya utabiri kwa sababu ile ilikuwa ipo, dunia kama kijiji kimoja, muda mrefu tu. Ila hatukuwa na macho au hisia za kuiona hivyo… Kwa mfano ukimwuliza simba aliyeko Manyara kuhusu simba aliyeko India habari zake *[kicheko]* – kwake kitakuwa ni kitu cha ajabu sana. Sisi wanadamu si tunajua wapo? Kwa hiyo athari za ugonjwa wa simba India sisi tunaweza kuzishughulikia *from a superior vision, from a superior outlook, right*? Kuwasaidia. Kwa hiyo kulikuwa na umuhimu wa dunia kuwa kijiji kimoja.

Ni yule mhusika Ahab wa *Moby Dick* ya Herman Melville akawa analitukana jua akiliambia: "Mimi namtafuta, mimi Bwana namtafuta yule nyangumi mweupe, namtafuta Moby Dick, wee una uhakika wa kumwona hapo alipo – *then tell me*!" Hakusema hivyo lakini maneno yake yalikuwa na maana ile kwamba hapa tulipo jua si linatuona, na yule nyangumi alipo linamwona lakini sasa mimi nina upungufu wangu wa kibinadamu. Lakini jua lingeweza hata kumwona na kuniambia kwamba yuko wapi huyu nyangumi.

Kwa hiyo yale ya Mungu yanakuja tena kwamba tunatamani angekuwepo *a superior being observing us, who could see* kijiji kimoja cha dunia. Hata hapo nyuma, hata miaka elfu moja

iliyopita, tamaa ya kuwepo kwa *superior being observing us* ingekuwepo ili aweze kuona huo ukijiji wetu mmoja. Hii ni dhana ngumu mno kuiepuka hata kama dhana ya kuwepo kwa *superior being* haiwezi kuthibitishwa.

Nafasi ya wanawake katika riwaya yako ni ndogo. Unawataja akina Clara, Roza na Emma (tz. ZZ Mzingo wa Vita II) ambao hapo baadaye tunaelezwa kwamba ni Clara Zetkin, Roza Luxemburg na Emma Goldman (tz. hapo IV). Walakini, wanawake hao hawachukui nafasi kubwa kama mashujaa wa kiume. Je, unafikiri mikinzano ya kifalsafa na ya kidini ilitokea kama ilivyotokea kwa sababu uwingi wa wahusika wakuu walikuwa wanaume?

Pale nyumbani kuna kitabu nakusudia kukisoma chote. Kinaitwa *Gender and Genius*[2], halafu kina sura inayoitwa *The Genitals of Genius*. Kimeandikwa na mwanamke mmoja wa Kiingereza. Nimekisoma kidogo tu, sijakisoma chote. Lazima nikisome. Ni kazi ambayo imejaribu kuchukua tatizo la hulka ya watu kuhusu *genius*. Watu wanasema *there is a male tone in 'genius'*. Mwandishi wa kitabu hicho anapinga tabia hii. Kwa mfano anasema kwamba mke wa Beethoven alikuwa hodari sana wa kupiga muziki kwenye piano. Lakini amefunikwa, kivuli cha Beethoven kilimfunika. Kumbe na mke wa Beethoven alikuwa *genius* wa kiwango chake. Sasa kwa nini *genius* inapozungumziwa mwanamke hapewi uzito mkubwa, hata kama atajitokeza kwenye *environment* ya magwiji?

Au tumchukue John Stuart Mill. Mke wake amechangia sana kwenye kazi zake, na ile *intellectual development* yake. Hata kwenye utangulizi wa zile kazi zake amemtaja, kwa mfano *On Liberty*, amemsifia mke wake kwamba amechangia sana. Lakini hakuna heshima inayotolewa kwa yule mwanamke. Inatolewa tu kwa John Stuart Mill mwenyewe. Tuendelee sasa kuhusu swali lako.

Hili ni suala la genius*. Lakini sasa ukiangalia suala la mikinzano na vita…?*

Vita yenyewe – vita ni ya wanaume, kwa muda mrefu sana. Nikizungumza vita, na nikizungumza mashujaa, nazungumza wanaume. Na ndiyo *tradition* ya wanadamu kwa muda mrefu sana. Mwanamke hutajwa kwa uzuri wake, hasa kwa Waingereza, kama anavyoukejeli George Bernard Shaw: Anazungumzia uzuri wa mwanamke wa Kiingereza ni ule unyonge-nyonge wake na ulimbwende wake, unaona? Siyo *strength.*

Lakini kulikuwa na wale wapiganaji wa Amazones...

Anaposifiwa huyo anasifiwa kwa ubaya. "Mbaya kama *amazone*" yaani…

Wanasifiwa kivita pia, kwa sababu walikuwa wapiganaji hodari sana kama watu wanavyosema. Lakini niliuliza kwamba kama unafikiri mikinzano ya kifalsafa na ya kidini ilitokea kama ilivyotokea kwa sababu uwingi wa wahusika wakuu walikuwa wanaume?

Si kwa sababu uwingi wa wahusika wakuu walikuwa wanaume ndiyo sababu ya kuwepo kwa ile mikinzano, ila mikinzano ilikuwepo, lakini wanawake hawakuhusishwa au hawakujihusisha nayo kwa wingi kama walivyojihusisha wanaume.

[2] Christine Battersby. 1989. *Gender and Genius*. London: The Women's Press.

Tofauti na riwaya ya* Nagona *ya Euphrase Kezilahabi, umeingiza zaidi nafasi na mchango wa Waafrika katika historia ya kitamaduni, kisiasa na kifalsafa katika riwaya yako. Umeyataja makundi mbalimbali ya Kiafrika kama Wayoruba, Wazulu, Waashanti, Wakamba, Wagikuyu, Wasambaa na Waluhya na mashujaa kama Fanon, Nkrumah, Lumumba, Mondlane, Machel, Cabral na Neto. Umekusudia nini katika kufanya hivyo?

Hata wao walishiriki. Kwa muda mrefu tunapozungumzia mtazamo wa mwanadamu, tunamtazama mwanadamu kwa kutotutambua sisi Waafrika *from the Western point of view*. Sasa siku hizi tunaanza kuitazama hata *from the Western and Eastern point of view. In fact* tunatazama *Western point of view*, halafu tunasema ngoja kwanza tunaangalia *Eastern point of view*. Hawasikilizi *the South American point of view, the Australian point of view,* na hawasikilizi *the African point of view*.

Kwa hiyo riwaya hii imeandikwa na mtu ambaye yuko Afrika, na hawezi kusahau kuwataja wale ambao wanahusika katika ile *point of view* yake ambayo ni *African point of view.*

Kuna sehemu chache tu katika riwaya yako zinazoonesha kwamba zina uhusiano fulani na mazingira ya Tanzania, kwa mfano kutaja kwamba kisiwa cha Nguu kiko karibu na kisiwa cha Mafia (tz. ZZ Duniani (I) II), au kutaja chakula aina ya kachumbari katika wimbo fulani (tz. ZZ Zirani IV). Tukiangalia uchache wa madokezo ya namna hiyo, je, ulifanya hivyo makusudi?

Kachumbari nimesema tu kama kuichangamsha lugha, na nisingesema *goulash* supu kwa sababu sijui *goulash* supu inavyotengenezwa. Halafu shetani anapenda kachumbari vilevile. *[kicheko kikubwa]* Lutzi, ukimpa kachumbari ataifurahia tu. *[kicheko kikubwa]* Lakini akienda Hungaria atapenda *goulash* soup, au siyo? *[kicheko]*

Kwa hiyo yuko universal.

Enhe, yuko *universal. [kicheko]* Sasa kisiwa cha Nguu nimekitaja kwa sababu gani? Ni *imaginary*. Kama umekikuta ulipokwenda Tanga basi bahati nzuri lakini ni *imaginary* katika hiyo riwaya. Siwezi kwenda mbali, ni *imaginary* wakati hapa jirani tunaweza kuwa na kisiwa kama hiki. Bahati nzuri tu kilihusikana na neno ‘Mafia’. Kuna ‘Mafia’ ya tafsiri ya Waitaliano, ile Mafia ya Sicilia. Lakini ‘Mafia’ maana yangu ni ile Mafia ya hapa Tanzania. Labda ungeniuliza swali la vita ya Mwendashari na Sharihaswa.

Lingalikuja hilo swali.

Sasa hilo lina uhusiano wa karibu sana na Tanzania, vita walivyoipigana Watanzania na Waganda. Lakini nayo pia nimeitumia *symbolically* kumaanisha ingeweza kutokea popote duniani.

Unajua nimefikiri nini? Nimefikiri unadokeza vita vya Ethiopia na Eritrea.

Na maana hiyo hiyo. Kwa sababu kichwani nilipoandika vita ya Mwendashari na Sharihaswa nilikuwa nafikiria vita ya Kuwait na Iraq.

Umedokeza hivi?

Mle hamna majina ya Kuwait wala Iraq. Kwenye hiyo riwaya hayamo, lakini nataka tu nikuonyeshe kwamba vita ya namna hiyo ndiyo iliyopo kokote kwingi. Kwa mfano vita ya Kuwait na Iraq ikasababisha msago wa watu wa Iraqi. Vita ya Uganda na Tanzania, vita hiyo unayosema, ya Eritrea na Ethiopia, vita ya Yugoslavia, Kosovo – si baadaye ikashushwa pale gharika ya mabomu na Marekani? Wamarekani wakaja wakashindilia mabomu pale? Kwa hiyo ile vita ya Mwendashari na Sharihaswa ni *symbolic*. Kwanza Mwendashari ni mtu anayeenda kwa shari, maisha yake ya shari. Na "Ukitaka shari, mimi ninayo haswahaswa" – ndiye Sharihaswa.

*Lakini kudokeza Tanzania ya wakati ule wa Mwalimu Nyerere na Uganda wa Idi Amin, kuwaita Mwendashari na Sharihaswa ki*spontaneously *inanishangaza.*

Aha. Ni kweli Nyerere alikuwa na kusudi jema kabisa. Lakini Idi Amin akavamia. Alipovamia sisi tukampiga. Sababu kulikuwa na kutoelewana na serikali ya Idi Amin kwa muda mrefu. Lakini pamoja na kwamba Idi Amin alikuwa Mwendashari na Nyerere alikuwa anajibu tu, ule uchokozi – mtu aliyekuweko pale Bukoba anapopatwa na adhabu ya vita ile, hajui hizo historia, hajui hizo *political issues behind*. Kuwait na Iraq, unapoisikia wewe kwenye magazeti au kwenye televisheni, ni tofauti na mtu, mzee kijijini pale Kuwait anaposagwa na mshindo wa mabomu! Anapoteketezwa na yale mabomu – yeye hajui hizo *politics behind the curtain*. Hajui.

Kwa hiyo yule mtu aliyekuweko kijijini anamwita Mwendashari Idi Amin, na Sharihaswa Nyerere. Yeye hajui kwamba Nyerere ana uzuri huu, na alikuwa na nia njema. Yeye anachukulia tu kwamba yule kamchokoza, na yule aliyechokozwa akapiga kwelikweli. Yeye hajui ubora wao au*, their moral qualities*, hazijui. Yeye anachojua ni kwamba ndege zilikuja zikawaua. Basi.

Je, ulipobuni nchi ya Bloblaha ulikusudia kuudokeza Uganda?

Kuna nchi ya Bloblaha ya Mwendashari, na nchi nyingine Porojoro ya Sharihaswa. Nchi hizi, sifa zao za kiuchumi, ni kwamba wale wengine walikuwa hodari sana wa kuongea, lakini hawajui kutekeleza. Halafu wale wengine walikuwa na neema ingawaje neema zilikuwa mikononi mwa wachache. Maana yake mojawapo ni *African socialist countries* ambazo zilikuwa zinaweza tu kuhubiri mambo ya mapinduzi na nini, lakini hawana lolote, kiutekelezaji. Lakini wale wengine wakaamua heri kuwa mabepari kabisa, na wakawa wanaendesha mambo yao kibepari. Kwa hiyo hao walikuwa wana shibe na wale wa Bloblaha waliishia kwenye bla bla.

Kwa nini umetumia 'Fuvu la Kichwa' kama jina la mahali fulani (tz. ZZ Mzingo wa Vita VIII)?

Katika riwaya 'Fuvu la Kichwa' inawakilisha Golgota. Yaani mahali Yesu alipouliwa. Ndiyo sababu ile jiografia ya kuzimu umbali wake umeelekezwa kwa kutumia umbali wa muda kutoka 'Fuvu la Kichwa'. Kama historia isemavyo *'before Christ (B.C.)'* na *'after Christ (A.D.)'*. 'Fuvu la Kichwa' imetumika kama kirejeo cha muda na umbali baina ya matukio ya kihistoria katika vita ile ya kwenye riwaya.

Katika ile *jiografia* ya kuzimu, kila kitu pale ni *symbolic*, kwa mfano kile kitivo cha Aquinus, ni kitivo cha hekima za Thomas Aquinus au msimamo wa kanisa la Katoliki kwa ujumla. Kuna sehemu inahusiana na majabali matatu ambayo ina maana ya Mekka au ngome ya Uislamu. Kwa hiyo kama kuna sehemu inaitwa 'Fuvu' inahusiana na kalenda ya sasa inayotambua kuanza kwa Ukristo kama kirejeo cha historia ya ulimwengu.

Ingawa maudhui ya riwaya yako ni mazitomazito, nafasi ya ucheshi pia imo, kwa mfano unapomchora Lusifa (tz. ZZ Zirani II 38) au mwishowe ambapo Lusifa anakiri kwamba amechoka na kazi ya ushetani na kuomba apewe kazi nyingine. Unaonaje wewe mwenyewe nafasi ya ucheshi katika riwaya yako?

Nimekusudia. Kwa sababu ni lazima kisa kifurahishe, mkasa uhuzunishe. Ni lazima watu wacheke. Na mwingine anachekesha, kwa sababu hiyo nafasi ya Lusifa kuitwa shetani, na Gabrieli kuitwa mtakatifu – ni *arbitrary*. Kwa hiyo ni kichekesho kwamba wajibu huo wa kimalaika unapozama sana kwenye nafsi za watu, wanaanza kuuhusisha kwelikweli na ubaya. Ziraili wanamwogopa, Gabrieli wanampenda na Lusifa wanamchukia. Kumbe ubaya ni kama katika ile sura ya *Motoni*, kwenye hotuba zile anavyosema maovu ya mwanadamu ni mengi, na yamekuwa ni ya muda mrefu. Kama tungemlaumu shetani, tutazidi kuonyesha upumbavu wetu sisi wenyewe. Kwa sababu mwovu siyo shetani – ni sisi wenyewe.

Fantasia inachukua nafasi kubwa katika riwaya hiyo vile kwamba sehemu nyingine zinafanana na ngano au fasihi ya kubuni ya kisayansi, kwa mfano jinsi unavyomchora Alalu (tz. ZZ Zirani III). Msukumo au kariha ya kuandika namna hiyo umeipata wapi?

Mimi nadhani fantasia iliyoniathiri zaidi kwenye hii kazi ni hizo mbili ya Dante na ya Milton. Hii fantasia ya ngano za kisayansi nimezisoma zamani sana, za kwenda kwenye mwezi, za kwenda katikati ya dunia, Jules Verne, *The Blue Planet*. Unajua mimi, ujana wangu, riwaya ilikuwa ni kimbilio langu. Kwa hiyo nilikuwa nasoma sana riwaya hizi. Kwa muda mrefu. Kwa hiyo sijui jinsi gani zimeniathiri. Sijui. Lakini kwa kukubali kwamba hapa katika kazi hii nimeathirika kwa kujihisia kabisa ni hizo mbili. *Fantasy* ya Dante ambayo hata hivi sasa bado si hodari sana kuielewa. Nimeipita kama mtu anayepita gizani, mengine anayachukua, mengine anayaacha. Hivyo hivyo.

Sasa kwa mfano kuhusu kulivyo huko mbinguni. Kulivyo mbinguni ni hiyo, inaweza kuwa ni kama kusoma mambo ya riwaya ya ki-sayansi: *Man on Mars.* Zaidi ni shetani ndio niliowachora: Nilivyokuwa mtoto – sijui hata hicho kitabu kama mnacho Ujerumani. Kwa sababu wazazi wangu mimi ni Waluteri. Kuna kitabu kiliitwa *Moyo wa Mtu*. Nilikisoma nikiwa mtoto wa miaka kama minane. Nilikuwa nakipenda sana hicho kitabu. Sasa walichora moyo wa mtu ulivyoathiriwa na Ibilisi. Kinaonyesha humo kwenye moyo wa mtu kuna mashetani wa aina nyingi. Kuna shetani wa uvivu, kuna shetani wa pesa, kuna shetani wa uasherati. Sasa sisi utotoni tulikuwa tunasema "Ah! Wewe unafanana na huyu!" Na tunalinganishana. Tena kiliandikwa kwa lugha yetu ya Kisambaa. Siyo Kiswahili. Nadhani ni kitabu cha Kikristo. Kwa hiyo kiko kwenye makanisa mengi. Kinaitwa *Moyo wa Mtu*. Na nina uhakika nakala ile iliyoko kule kwetu ni tafsiri. Kwa hiyo bila shaka iko ya Kijerumani. Wamemchora mtu, ha-

lafu na moyo wake umechorwa kama ndiyo tumbo. Wanamchunguza zaidi mle ndani, kwamba kwenye moyo wake mna shetani yupi anayetawala katika nafsi yake.

Ukitazama katika ile sura inayozungumzia maandalizi ya kwenda vitani. Wanakuja aina kadhaa za shetani, anakuja Beelzebabu, anakuja nani, Asmodeus na kimada wake Lilitu. Hizo ni baadhi za viashiria vya shetani – fantasia hii imeathiriwa na ile kumbukumbu ya wakati ule.

Kejeli na tashtiti pia zinachukua nafasi isiyo ndogo katika riwaya yako. Kwa mfano tunasoma hoja au swali lifuatalo: Je, kuumbwa kwa binadamu mwingine kutafanikiwa zaidi (tz. ZZ Sherehe II)? Unaonaje nafasi ya kejeli na tashtiti katika uandishi wako na katika fasihi kwa ujumla?

Dawa nzuri ya utata ni kicheko. Kwa hiyo ukicheka hata lile lililokuwa gumu mwishoni unaliona "Ah! Basi tu Bwana, limeshapita." Sisi Waafrika, *infact* ni sisi Watanzania, kuna kitu kinaitwa utani. Kwenye utani hata ukiwa na msiba wanakuja watani hapo wanaanza wanazungumza mambo mengine ya pembeni kabisa. Wanaanza kucheka na hatimaye hata ule uchungu unatoweka.

Kwa hiyo kicheko ni kitu kizuri, ni *tonic* ya maisha. Kwa hiyo kejeli na ucheshi katika sanaa ni kitu kizuri, kwa sababu kinamfanya msomaji au kwa ujumla mwanadamu ayatazame mambo kikejeli. Ni *absurd* kuangalia kwamba *you are born and you live only fifty years and then you die off, or one hundred years, and then you die* – usipocheka *you are in trouble*! *[vicheko]*

Mwishoni mwa sura ambapo Zirani anafunzwa katika kambi ya mashetani, yanarudiwa yaliyoelezwa kabla ya hapo (tz. ZZ Zirani IV). Kwa upande wa kisanaa haivutii sana kama sauti ya msimulizi inamweleza msomaji maudhui yaliyosawiriwa kabla. Kwa nini uliiandika hivyo?

Zirani alikuwa amepelekwa kule kwa makusudi ya kujua kinachoendelea kule kwenye kambi ya mashetani. Shetani akimweleza Zirani pia anakueleza wewe, na ananieleza mimi. Yule Zirani pale anamwakilisha mwanadamu. Na shetani anamwambia mwanadamu anavyowaona mashetani, na mashetani wanavyomwona mwanadamu. Kwa hiyo baada ya yale mambo ambayo mashetani walikuwa wanamhubiria, kila mmoja anakuja anamwambia mambo kwamba wewe uko hivyo, uko hivyo, uko hivyo, na wewe ulipewa sifa ambazo huzistahili kabisa. Kwanza hapakuwa na haja ya kuwa na mtu kama wewe. Baada ya pale, ni kama *summary* tu. Yale yote yaliyoongelewa sehemu mbalimbali *summary* yake ni hii hapa. Yule Zirani anaitolea muhutasari. Lakini vilevile ile *summary*, kwa sababu kila mmoja kasema maoni yake ki-vyake, inataka ijengwe ujumla wa hoja kuhusu mambo mbalimbali. Jinsi Zirani alivyoelimika na kubadilishwa na hoja hizo. Kwamba amepevuka kwa kiwango gani katika kuwepo kwenye kambi ile.

Kwa hiyo kusudi lilikuwa hilo. Kwa msomaji ambaye anataka kupata ile burudani tu, anaweza kukereka. Lakini kama anafuatisha umantiki wa hoja na matukio kutoka mwanzo,

ule muhutasari ni muhimu kuonyesha kambi ile ilivyochangia katika kumjenga mhusika Zirani.

Katika sehemu kadhaa za riwaya hiyo tunakuta mashairi na nyimbo (tz. ZZ Matukio 5; Mbingu 10; 12; 15; Ziraili 28; Zirani 42-43; 52; Motoni 90-92; 109-110; Duniani (I) 133-135; Mzingo wa Vita 145; 153; 156-157; 178; 183-184; Mtingisho wa Vita 187-189; 194-196; 200-201; 205-206; Kiama 212-218; 221-223; 226). Ulikusudia nini kwa kuingiza aina hii nyingine ya matini katika nathari?

Ushairi – hii *epic* ya *Ziraili na Zirani*, ukiangalia sehemu nyingi sana, ingawaje ziko katika nathari, lakini ukizikata unapata mashairi pia. Kusudi ni kwamba kwa kuwa ni *epic*, visifa vya jambo lililotokea ni lazima viwe na vichocheo vya lugha. Lugha iwe na hamasa, iwe na vibwagizo. Ndiyo inakuwa ile sanaa ya ki*epic* inazidi kuimarika pakiwa na ushairi kama huo.

Ukieleza kwa nathari ya kawaida tu, masimulizi yanakosa msukumo, yanaanza kuchosha. Lakini hizi nyimbo nyimbo, vibwagizo vibwagizo vinasaidia kuipa ule msukumo wa ki-*epic*. Ningekaa chini ningeiandika kama utenzi. Lakini siku hizi watu wameanza kuchoka kusoma *utenzi.* Kwa hiyo ile hadhira yangu isingekuwa kubwa kama hivi sasa ambavyo nimeviweka vile vibwagizo hapa na pale. Kwa hiyo ilikuwa tu ni *approach* ambayo niliona ingeongeza ule msukumo wa kisanii.

Kwa mtazamo fulani tunaweza kusema kwamba Ziraili na Zirani inaweza kusomwa kama maendelezo ya riwaya fupi Nagona ya Euphrase Kezilahabi. Katika riwaya zote mbili, falsafa inayojitokeza zaidi ni falsafa ya udhanaishi. Kwa mfano Ziraili anatamka yafuatayo: "Wanadamu wanazaliana mno na wanachelewa kufa. Karibuni dunia itafurika" (ZZ Ziraili 31).

Kuhusiana na hilo nilipewa hoja na mtaalam wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Alisema ile dhana ya dunia kufurika na wanadamu kuzaliana mno – anaiona ni ubeuzi, kwa sababu tatizo la msingi la binadamu ni ugawaji mali usio sawa duniani. Ugawaji mali duniani ungekuwa sawa, haingekuwa shida kwamba tuko binadamu milioni sita au saba au nane. Unaonaje suala hili?

Kwa kweli hili sikubaliani naye. Tutake tusitake, tukimheshimu Malthus, dunia inaweza kujaa. Si unajua *Malthusian theories*? Kwamba *a certain system* inaweza kuji*tosheleza* kwa muda fulani tu, lakini kama *population* inaongezeka mno uzalishaji wa mahitaji ya ile *system* utafika *optimal limit*, ambayo ile *population* ikizidi pale itaiondoa ile *optimum*, ile *balance.* Ile *equilibrium* itakuwa *distorted*, hakutakuwa na *equilibrium*. Kwa hiyo ile *population* jinsi inavyoongezeka itaharibu uwiano, itasababisha *imbalance* ya mahitaji na kiwango cha kuyatosheleza. Hapo ile *system* yenyewe italazimika kujipanga upya, vinginevyo ile idadi ya watu ni lazima ipunguke ili ile *system* iweze ku*dumu*. Dunia ina mipaka. Ukisema haiwezi kujaa ni kama isingekuwa na mipaka – hapo tungeweza kusema hivyo. Lakini dunia ina mipaka. Ni hii anga, na hii ardhi. Kwa hiyo kujaa inajaa.

Sasa hivi tatizo la mwanadamu kujaa – dunia haitajazwa na watu tu wenyewe. Pia itajazwa na matumizi yake, na vitu anavyotoa, anavyoharibu. Hata kule kukata miti, kwa sababu tuko

wengi, zamani walikuwa hawakati miti mno, lakini sasa tumeongezeka kwa hiyo miti inazidi kupungua. Au magari kutoa moshi wenye sumu kwenye mazingira ya dunia. Kwa hiyo kujaa dunia imejaa. Sikubaliani naye kwamba dunia haijajaa.

Ndiyo. Sasa tukiyachukulia maoni haya synchronical *bila kuangalia mbele. Labda amekusudia hivyo. Tukisema "Sawa, sasa hivi tuko milioni sita, na tatizo la msingi zaidi ni ugawaji usio sawa wa mali..."*

Ahaa. Hiyo kauli ingekuwa na neno zaidi. Yaani kwamba tatizo la msingi zaidi *kwa sasa* siyo kuwepo kwa wingi wa watu. Ila tatizo la sasa hivi la msingi ni ule ugawaji wa kilichopo. Hapo nakubaliana naye. Hilo ni neno zaidi, kwamba ni *relative sasa*.

Eee. Lakini mtaalam huyu alikusudia zaidi kuukosoa udhanaishi kwa ujumla, kwa sababu....

…akikosoa udhanaishi, kama hii ndiyo *argument* yake kwamba ni matokeo ya ugawaji potofu wa mali za dunia, sio uwingi wa idadi ya watu – hiyo mimi naikataa kwa sababu *phenomenon* ya udhanaishi haisababishwi na dhiki au mgawanyo potofu wa mali peke yake. *Phenomenon* ya udhanaishi inahusiana na mwanadamu kujitambua hatima yake, upeo wake na kadhalika. Hoja kwamba wingi wa watu hautafika mahala ambapo tutashindwa kuongezeka jibu lake ni la kisayansi na halina haja ya kubishana.. Nenda tu kwa mfano Hongkong. Kisiwa kimejaa. Kutafika mahala ambapo uwingi wa watu utaathiri maisha yao hata kama wakigawana sawasawa majumba na vitu vilivyomo.

Unaonaje athari ya riwaya ya* Nagona *kwa uandishi wa* Ziraili na Zirani*?

Sikuwa nimeisoma hiyo *Nagona*. Nimeisoma juzi.

Mojawapo ya tofauti baina ya riwaya hizo mbili ni kwamba* Ziraili na Zirani *inachunguza historia ya falsafa kwa undani zaidi. Tofauti nyingine ni kwamba sauti ya masimulizi inasikika zaidi kumweleza msomaji ujumbe. Kwa ujumla wewe mwenyewe unaonaje 'udugu' baina ya riwaya hizo mbili, au labda unasema hamna 'udugu' wowote?

Udugu unaweza uwepo, unaweza usiwepo. Kwa sababu hata hiyo *Nagona* nimeisoma juzi, kuna kwingi ambako ninakwama. Nagona ni riwaya ngumu. Ni jamii ya riwaya za kidhanaishi kama *The Fall* ya Camus au *Nausea* ya Sartre.

Epic ya *Ziraili na Zirani,* kusudi lake ni kuonyesha kukua kwa mtazamo wa mwanadamu, kukua kwa kosmolojia ya mwanadamu hadi alivyofika kwenye kiwango cha *dialectical materialism.* Lakini pia maoni ya wahusika ambao pia wananiwakilisha mimi kama mwandishi, maoni ya wahusika mbalimbali kuhusu hizo ngazi, halafu hatima ya maoni yangu mimi mwenyewe imejitokeza zaidi kwenye hizi sura za mwishomwisho ambazo anaota ndoto.

Kwa hiyo *Nagona,* nilivyoisoma, ninapata hisia kama nilivyosoma *Nausea* ya Sartre. Kwa sababu anaanza gizani, anaishia gizani. Na lile giza limo, kote liko giza, kwa sababu kila wakati anaanza na sentensi "Sijui nilikuwa wapi na nilikuwa si-, nilikuwa si-...", yaani kuna ile *vagueness.* Ni nyingi mno. Kwa hiyo hamna *light.* Hamna *light* kwenye *Nagona.* Hakuna

mwanga. Ni giza kutoka mwanzo mpaka mwisho. Si giza tu kwa macho, ni giza hata kwa zile *concepts* zilizokuwa mle ndani.

Isipokuwa kuna 'askari wa mwanga' kama motifu...

Eee, halafu tena hata hao 'askari wa mwanga' wanapojitokeza hawana nguvu ya kutoa mwanga wa kutosha. Wale 'askari wa mwanga' wenyewe, *concept* yake, walivyowekwa mle, wanakuwa wenyewe pia ni *abstract*, na ile *abstractness* yake inazidi yenyewe kuongeza giza tena.

Lakini huyu mhusika msimulizi anapata mwanga mwishoni mwa Mzingile*, kwa hiyo ingenivutia sana tukiweza kuzungumza juu ya* Mzingile...

Mzingile sikusoma. Lakini ninalosema ni kwamba: mimi nilivyosoma *Nagona*, naona hili gizagiza na *vagueness* na utusitusi. Kwa sababu liko kutoka mwanzo mpaka mwisho. Nadhani pengine mwandishi alikuwa anataka atuonyeshe kwamba maisha ni utusitusi, ni *vague*, ni kama ilivyo kwenye *Nausea. Nausea* yenyewe, ingawa niliisoma nilipokuwa kijana, lakini nataka niisome katika ukubwa wangu. Pale ujanani niliipenda tu kwa tabia za kijana kujaribu mambo magumu lakini kusema kweli nilielewa kidogo mno. Ila niliona hilohilo giza. Kwa hiyo hata kwenye *Nagona*, ule utusitusi unaanza kutoka mwanzo mpaka mwisho. Sasa ndiyo kusudi la mwandishi la kutuonyesha ule utusitusi? Kwamba maisha ni utusitusi?

Kama ni hilo, ni vizuri tu, hamna tatizo. Mimi, kusudi la *Ziraili Na Zirani* ni mwanga, kutoka mwanzo kusudi kila ukiangalia matukio yanaelekea kwenye mwanga, kusudi ni ku*enlighten* msomaji...

...eee, imekuwa na hiyo spirit *ya* enlightenment...

... eee, ile *spirit* ya ile *novel* ni ku*enlighten.* Ni kutoa mwanga. Hata ukikuta na Zirani, kazi yake anabishana alipoenda motoni, gizani kule, kusudi ni kutoa mwanga kule gizani. Hata wanapokaa kwenye mkutano wakijadiliana, wale wanapoleta *mystification of life* kwa kutumia *religion*, wanatokea akina Voltaire wana*enlighten them.* Kwa hiyo hata unavyoenda kooote, kusudi ni kuleta mwanga. Sasa *that is the biggest contrast between Nagona and Ziraili na Zirani*. Kwa sababu kimoja kinaeleza giza, kingine kinaleta mwanga.

Jambo ambalo linajidhihirisha katika riwaya yako ni kwamba kitabu cha 'Akirikifuk' kinadokeza riwaya ya kinjozi ya Kufikirika (1967 [1946]) ya Shaaban Robert. Kwa nini umedokeza hivyo?

Hiyo nimeipenda, hili jina la *Kufikirika*. Kwa sababu *Kufikirika* ni *abstract world* katika riwaya ya Shaaban Robert. *Ziraili na Zirani* haizungumzii yaliyomo kwenye ile riwaya ya Shaaban Robert, ila nimetumia jina la kitabu hicho cha Shaaban Robert kwa heshima na pia kwa dhana kwamba mambo ya mbingu ni kufikirika tu. Ndiyo sababu wanapopambana na jambo gumu, ndiyo ni yaleyale kuhusu *light*, akitamka tu 'Akirikifuk!' linatatuliwa.

Mwanga ni ile elimu kwamba ugumu huo waliokumbana nao ni dhana tu, *it is not true*, hakuna mbingu. Kwa sababu hata yule shetani anavyokuja akawa anachezacheza pale nje ya

ngome na kufanya fujo huku akiimba nyimbo zake, kiongozi wa kambi akasema "Tamkeni 'Akirikifuk'!" Walivyotamka lile lango lililokuwa linakataa kufunguka, likafunguka. Maana yangu ni kwamba: dunia au mwanadamu atakapotazama hizi *mystifications*, atakapozitazama kwamba hizi ni dhana tu, ni kufikirika, ndipo hapo atakapopata mwanga.

Vilevile unadokeza mara kadhaa Magriots yaani waimbaji wa kijadi wa Kiafrika (tz. Motoni II; Mzingo wa Vita VIII & Mtingisho wa Vita III), halafu na Enugu, na sehemu ya matini ya Christopher Okigbo. Umekusudia nini katika kufanya hivyo?

Yule kasisi wa Enugu, *actually* siyo Christopher Okigbo mwenyewe, ila ni mtu aliyevutiwa na ule utenzi wa Christopher Okigbo. Kwa nini ule utenzi? Ni kwamba hizi dini nyingi zinaambatana sana na *utenzi.* Halafu zinaeleza kitu kilicho ndani kwa kutumia viashiria (*symbolism*). Pia utenzi wa Christopher Okigbo ukiusoma pale unapotoka kwenye *Distances* – kuna mahali ambapo anakutana na Mungu, akawa sasa anakata kucha. Ni ngazi ya juu kabisa.

Ni kama ulivyo kwenye *Kubla Khan* ya Coleridge: Anapofika kule ndani kwenye zile kasri, na kadhalika. Ile ngazi ina maana ni *search for the truth.* Kuwepo kwetu kuna asili yake? Kwa hiyo nimeuhusisha ule utenzi tu, kwa sababu imani zote zina uhusiano na hiyo kiu ya kuupata ukweli, ingawaje ni ukweli-dhanifu. *The phenomenal world* tunayoiangalia, jinsi inavyozidi kuwa fumbo inavyozidi kuwa *poetic*. Au kutatanika kwetu kunatufanya tuzue lugha ya kishairi.

Kwa hiyo ndiyo sababu nukuu kadha za washairi zimehusishwa mle na mimi mwenyewe lugha ya hiyo hekaya nimeikoleza kwa ushairi.

Naomba tuangalie mfano wa wimbo anaouimba mghani wa Enugu (tz. ZZ Mzingo wa Vita III 199)...

…hii ni *elegy*. "Rambirambi, midomo imepasuka kwa rambirambi..." *[ubeti wa mwisho wa huu wimbo]*. Kiswahili chake tungeweza kusema ni wimbo wa rambirambi. Lakini kote kule alikuwa anatabiri kwamba ninyi huko mnakoenda mtaenda kupambana na mwanga. Mtaenda kupasuliwa, mtaenda kupambana na mwanga. Infact huyu ndiye *the prophetic figure* kwenye hii riwaya.

Siyo Voltaire.

Voltaire? Voltaire pia ni *prophet* kwa maana ya kutabiri, yaani kuona kilicho mbele kabla hakijakufikia. Lakini pia kuna prophecy kwa maana kama ile asemayo E. M. Forster kwenye *Aspects Of The Novel*, ambayo, kama nilimuelewa, ni ile ngazi ya uandishi yenye mtiririko wa masimulizi unaoelekeza ujumi wa msomaji kuweza kutarajia au kutabiri hatma au ujumuisho na ukamilisho wa *plot*. Nyimbo za huyu mghani wa Enugu ziliwaandama kina Zirani hadi zilipoishia kwenye "rambirambi". Kwa hiyo *the prophetic figure* humu ndani ni huyu kasisi wa Enugu.

Sura mojawapo inazungumzia kisiwa cha kubuni cha Nguu ambapo kuna mradi wa kisiri wa kuwanyima watu viungo vyao kama vile figo na kuviuza na kuvisafirisha nje ya nchi (tz.

ZZ Duniani (I) II). Mada hiyo inamkumbusha msomaji riwaya ya* Vipuli vya Figo *(1996) ya Emmanuel Mbogo. Umedokeza hivyo makusudi?

Sijaisoma hiyo riwaya. Lakini kipindi fulani kwenye magazeti na redio walikuwa wanazungumzia kuhusu jambo hilo. Watu walichukua viungo vya figo. Bangladesh walikuwa wanaziuza, figo zao na viungo vyao vingine.

Ile imeanza na sura za *Duniani (I)* na *Duniani (II)* – maana yangu ni kwamba vita ya hii riwaya ilikuwa inapiganika huko mbinguni, lakini tukachukua *excursion* duniani. Tukarudi kwanza duniani kuona kinachoendelea huko ni kipi. Sasa kinachoendelea ni kitu kama vita ya Mwendashari na Sharihaswa. Kuna vita. Watu wanauana kwa sababu ya tamaa za mali, mamlaka na viburi vya viongozi wao, lakini watu wanateketezwa. Hiyo ni aina moja ya maisha wanayoishi wanadamu. Aina ya maisha ambayo inaathiri imani zao.

Halafu vilevile ikaja *excursion* nyingine: maendeleo ya sayansi, na jinsi kunavyokuwa na viwanda vya kutengeneza mashine za kuteketeza wanadamu. Makampuni makubwa sana ya Marekani yanauza silaha duniani kote. Kusudi ni nini? Kusudi si kujiua tena? Kuua wanadamu walewale? Sasa hii ni biashara ya kishetani pia. Shetani *in the real sense* hasa ya shetani, mtu mwenye uovu uliokithiri kwa nia ya kuuangamiza u-anadamu. Siyo shetani wa Kibibilia au wa Kiislamu ambaye uovu wake hasa ni wa kumkosea Mungu, sio uovu wa kuukosea u-anadamu.

Maendeleo ya sayansi – utafika muda ambao tuko kwenye kipindi ambacho tuna *a serious problem facing us*. Baada ya kuuana sana tumebaki mimi na Luti. Tunakuta mahala ambapo hatuwezi kuwepo wote. Sasa tuchague mmoja abaki. *[kicheko]* Sasa abaki Luti au mimi? *[kicheko]*

Nani atashika bao la mwisho tukizama?

Eee, sasa ndiyo hapo sasa. Ukiangalia kwa mfano sasa hivi tunapozungumzia kuhusu *the global world*, ni kwamba kutafika muda ambao tutasema wabaki nani. Wabaki nani? Na nani wapate, nani wafaidi neema za dunia? Ni nani? Ndiyo hiyo hiyo ngazi tunayofika, kwa hiyo ndiyo hapo bado tunapofika kwamba mwanadamu atatumia mwanadamu mwingine kumtengeneza mwenzake asife, aendelee kuishi. Sasa huyu ambaye anatumiwa amtengeneze yule ana upungufu gani?

Ndiyo sababu mle kwenye jaribio la kisiwa cha Nguu ilibidi wawaharibu wale viumbe nafsi zao kwa kuharibu ubongo. Waliwaharibu nafsi zao, ili wapungue ule uanadamu wao, ndiyo waweze kutumia vile viungo vyao kwenye mahospitali ya ulimwengu. Lakini *there is a very critical philosophical question there* kwamba itatokea nini wakati mwanadamu atakapojinadi mwenyewe, atakapo*commercialize himself*? *What will happen*?

Aidha, imo miingilianomatini mingine katika riwaya hiyo. Unawadokeza akina Shelley, George Bernard Shaw, T. S. Eliot, Christopher Okigbo – umeshamtaja – na Ayi Kwei Armah. Je, tunaweza kuchukulia kwamba hao wamekuathiri zaidi katika uandishi wako?

Kwa kweli siwezi kusema aliyeniathiri ni yupi. Ni *broad reader*. Nasoma kwa mapana na sichagui. Ila utenzi wa Christopher Okigbo nimeupenda sana. Mimi nilivyokuwa mwaka wa kwanza Chuo Kikuu, nilikuwa nimeuchora huo utenzi. Sijui michoro yangu imepotea wapi. Ile *Labyrinths* nimeuchora kutoka shairi la kwanza mpaka la mwisho. Jinsi ile hisia inavyonipata ndivyo nilivyoichora kwenye karatasi. Kwa hiyo nimeupenda ule utenzi wake. Ndiyo sababu umeuona unajitokeza sana hapa kwenye ile riwaya. Ameniathiri huyo, kishairi. Nakubaliana na hiyo. Naye Christopher Okigbo aliathiriwa na T. S. Eliot niliyemsoma pia.

Kwa hiyo naye T. S. Eliot kwa kiasi fulani ameniathiri. Hata yeye, kwenye riwaya nimem-*quote.* Kuna mahala ambapo anacheka kwamba "Ah, ninyi mmekubali mambo ya kuabudu miti, na mizimu na majoka, sasa mnaona mlikoishia".

Shelley nimemsoma kwa kiwango kidogo lakini ile *elevated language* yake inanifurahisha. Siwezi kusema kwamba ameniathiri labda ungesema S. T. Coleridge.

Na huyu Ayi Kwei Armah – hoja yake kuhusu imani, hasa katika *Two Thousand Seasons*, kwamba tulipotoka na kwenda pembeni mwa njia yetu. *There was a way*, hapo mwanzo tulikuwa na njia, mwelekeo, lakini tukaenda pembeni. Na upotofu huo ukatuathiri sisi Waafrika. Na yeye kwa kweli anazungumzia kuhusu *position* ya Afrika.

Na G. B. Shaw?

G. B. Shaw – nimesoma tamthilia zake nyingi. Ameipa tamthilia sababu, kama Tolstoy alivyoipa riwaya sababu. *They are didactic novels*, kama hizo plays za G. B. Shaw. Zote ni *didactic*, *they are educative, they are giving light.* Kwa hiyo nampenda sana G. B. Shaw.

Swali lifuatalo linahusu lugha unayoitumia: kwa nini ulianza kuandika kwa Kiingereza, halafu ukaacha na kuandika kwa Kiswahili?

Kwa sababu ya heshima unayopata ukiandika Kiingereza wakati ule. Unajua, uandishi wa Kiafrika uliimarishwa sana na *Heinemann*, katika *African Writers' Series.* Na sisi wakati ule tulivyokuwa vijana ukizungumza riwaya hasa kama unazungumza kifasihi – siyo kusoma tu ya James Hadley Chase na Ian Fleming. A-a. Lakini ukisoma hizi za fasihi zinazohusiana na masuala ya Afrika ni za *African Writers' Series*. Sasa zile ni riwaya za Kiingereza. Kwa hiyo kwa sababu tumezisoma wakati ule kwa uwingi sana, basi nikaona ah!, napata *prestige* nikiandika Kiingereza. Lakini baadaye ndiyo nikaona kwamba niko *mwepesi* zaidi nikiandika Kiswahili. Nikiandika kwa mfano kwenye *Ziraili na Zirani* – kazi hii nimejaribu kuitafsiri mpaka sasa hivi sijaweza. Kwa sababu bado Kiingereza ni kigumu.

Lakini si wakati ule ulipokuwa mwandishi hapa Tanzania, uwingi wa waandishi, tuseme asilimia themanini au zaidi, waliandika kwa Kiswahili tayari? Hii ndiyo sababu ya kukuuliza swali hili, kwa sababu wengi wenzako wameanza moja kwa moja kuandika kwa Kiswahili.

Mm. Ni hilo hilo suala la *prestige* ambayo ni *false prestige, of course*. Lakini niliona ni heshima zaidi kuandika Kiingereza. Hii ilikuwa ni kasumba tu. Ilikuwa kasumba. Naona ni

vizuri zaidi sasa hivi naandika Kiswahili. Lakini vilevile nyingine ni kwamba ile *audience* yako wakati ule ni kubwa zaidi ukiandika Kiingereza kuliko ukiandika Kiswahili.

Swali la mwisho, halafu tutashusha pumzi! Nafikiri umeshajibu sehemu. Katika fasihi ya kiulimwengu, unawapenda waandishi gani zaidi?

Ni ngumu kuchagua kwa sababu kila mmoja ana utamu wake. Lakini mmoja katika uandishi wa michezo ni George Bernard Shaw. Na yeye ameathiriwa sana na Nietzsche. Kwa hiyo nafuata huo huo mkondo pia – kumsoma Nietzsche, *the philosophical input* ya Nietzsche. Nawatumia jinsi ninavyo*tackle arguments* ninazoziandika kwenye *Ziraili na Zirani*. Ingawaje mimi mwenyewe nina hoja zangu na muundo wangu wa uandishi.

Katika *ushairi* – Coleridge, na Christopher Okigbo, na T. S. Eliot. Nawapenda.

Kwenye upande wa riwaya – ni vigumu kusema. Kwa sababu gani? Ni nyingi, na zote, kila moja ina ladha yake. Hivi sasa nasoma *The Brothers Karamazov*. Nilipenda sana *Crime and Punishment*, na *character* ya Raskolnikov. Ukimtazama Zirani – ingawaje Raskolnikov alikuwa ametenda *crime*, na alikuwa anakimbiakimbia – lakini unajua *character* ya Raskolnikov ndiyo iliyopo kwenye *The Outsider* ya Camus, ndiyo iliyopo katika *Native Son*, Bigger Thomas, na ndiyo hiyo hiyo iliyoko kwenye – juzijuzi nilikuwa nasoma *Resurrection* ya Tolstoy. Ndiyo hiyo hiyo. Naiona ni *character* ambaye ni symbol of *the modern young individual* na jinsi anavyoathirika na mabadiliko ya maisha. Kwa hiyo Zirani ingawa si kwenye mambo ya *crime*, lakini ana sifa hiyo. Katika riwaya zangu zote nadhani nina mhusika wa aina hiyo.

Lakini Albert Camus nampenda sana, hasa kwenye hizo riwaya zake mbili za *The Plague* na *The Stranger*. Sasa huko nyuma, nilikuwa nampenda D. H. Lawrence. Kwa hiyo siwezi kusema ni yupi nampenda zaidi. Halafu juzijuzi hapa nimemsoma Hermann Hesse. Ah! *He is such a sweet writer.* Mimi natafuta riwaya nyingine. Ninayo moja niliikuta kwenye hizi *book stores* za barabarani. Sasa natafuta za Thomas Mann na za huyu Hermann Hesse.

Umesoma Siddharta*?*

Eee, *Siddharta*, nimeisoma. Ninayo nyumbani hiyo.

Na ya Thomas Mann umesoma ipi?

Sijapata ndiyo naitafuta. Hermann Hesse, Bwana... Halafu, ukisoma Hermann Hesse, yaani kila nikiwa nina maudhimaudhi tu hivi – ile ni riwaya na imeandikwa kinathari, lakini mimi naisoma kama *poem*. Kwa hiyo nikiwa na maudhimaudhi tu ninaenda tu nasoma ile. Ni nzuri sana.

Inatuliza sana.

Ah! Inatuliza sana moyo aisee. *[Vicheko]*

Nashukuru sana. Nashukuru sana kwa subira yako kubwa sana. Nimejifunza mambo mengi sana.